

# **Stadi za Kutumia Kamusi: Haja ya Kufundisha Matumizi ya Kamusi Shuleni**

*James S. Mdee  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

## **1.0 Utangulizi**

Lengo la makala ni kujadili stadi za kutumia kamusi walizo nazo wanafunzi wa sekondari ili kuona ni kwa kiasi gani wanahitaji kufunzwa kutumia kamusi. Makala haya yanatokana na utafiti uliofanywa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule mbili za sekondari, Mringa iliyoko Arusha na Eckenforde iliyoko Tanga.

Usuli wa utafiti huu unatokana na mitazamo tofauti kuhusu matumizi ya kamusi ambayo mtafiti alikumbana nayo wakati wa kuuza kamusi katika shule za sekondari. Baadhi ya walimu hasa wa Kiingereza huwakataza wanafunzi wasitumie kamusi kwani wanadai kuwa itawalemaza wasijifunze kudadisi maana ya maneno kutokana na muktadha wake. Walimu wengine waliona kuwa ni muhimu kwa wanafunzi kutumia kamusi ili wajifunze kujitegemea kutafuta maana za maneno wanaposoma matini bila kumtegemea mwalimu wanapokutana na maneno magumu. Mitazamo yote miwili ina ukweli fulani japokuwa sio ukweli wa kuukataa mtazamo mwingine. Ni muhimu kumfunza mwanafunzi kujua jinsi ya kudadisi maana za maneno kutokana na muktadha kwani sio kila neno hupatikana katika kamusi, na hata kama lipo katika kamusi sio maana zote huwa zimeingizwa katika kamusi. Hali hii hudhihirika zaidi katika lugha ya mazungumzo ambapo maneno mengi huundwa, na hata maneno ya kawaida hupata maana mpya ambazo hazipo kwenye kamusi. Lakini kupinga kutumia kamusi kwa sababu ya kutaka kudadisi maana kutokana na muktadha ni kutokuelewa kuwa kamusi ina taarifa zaidi ya maana, taarifa ambazo hazipatikani kwenye muktadha peke yake.

## **2.0 Stadi za Kutumia Kamusi ni Nini?**

Stadi za kutumia kamusi ni maarifa ambayo mtumia kamusi anayahitaji ili kutafuta neno katika kamusi au kutafuta taarifa anayoitaka kutoka kwenye kamusi, mathalani matamshi, vibadala (vya lahaja ya lugha), maana, taarifa za kisarufi, (kategoria ya neno, minyambuliko ya vitenzi, upatanisho wa kisarufi, miambatano ya maneno), etimolojia, tungo funge, mifano ya matumizi, hadhi ya maneno kama vile maneno yatumikayo katika lugha ya mitaani (simo) mathalani lugha ya vijana, wanawake, wanafunzi, makuli, askari n.k., mazingira ya matumizi ya maneno, yaani maneno yawezayo kutumika katika mazingira mahsusi kama vile mazingira rasmi kwa mfano shuleni, mikutano ya hadhara,

mahakamani, ofisi za serikali na makampuni au mazingira yasiyo rasmi kama vile miongoni mwa marafiki, ndugu n.k. Isitoshe stadi ya kutumia kamusi humpatia mtumia kamusi maarifa ambayo humwezesha kutambua aina tofauti za kamusi na taarifa ambayo kila kamusi inayo.

Hii ni muhimu kwa sababu hakuna kamusi inayoweza kukidhi mahitaji yote ya kutumia kamusi ya kila mtu. Aidha hakuna kamusi iwezayo kuwa na maneno yote ya lugha. Hata zile kubwa zenye vidahizo 400,000 - 500,000 kama vile Kamusi ya Kiingereza ya Oxford yenye majuzuu 12 (1885 – 1928, au ile ya Webster NID 1962 hazina maneno yote. Hii ndio maana Kamusi ya Kiingereza ya Oxford imekuwa ikitungiwa majuzuu ya nyongeza ili kuingiza msamiati mpya ambao haupo katika matoleo yaliyotangulia. Sababu hii ndiyo hufanya kamusi mpya zenye kulenga watumiaji wa elimu, umri, lugha au taaluma mahsusi kutungwa kila wakati. Hali hii inaonyesha kuwa kila kamusi ina upungufu fulani ambao hujaliziwa na kamusi nyingine. Taarifa hii ni muhimu kwa mwalimu wa lugha kwani humwezesha kutafuta kamusi itakayofaa mahitaji ya wanafunzi wake.

Stadi ya kutumia kamusi humwezesha mtumia kamusi kufahamu sehemu kuu za kamusi, mpangilio wa vidahizo na jinsi taarifa anuwai za leksikografia zilivyoingizwa katika kitomeo. Ufahamu huu ni muhimu kwa sababu taarifa hizi huingizwa kwa misimbo ambayo ni herufi au kifupisho cha neno, tarakimu, alama za uandishi kama vile mkato, nukta, nukta na mkato, nukta mbili n.k. Kila msimbo huwakilisha taarifa maalumu ya leksikografidia katika kamusi. Hata chapa nayo huwa na maana pia katika kamusi, mathalani neno lililochapwa kwa herufi nzito au herufi za italiki huashiria hadhi ya neno au maneno hayo ikilinganishwa na yale yenye chapa ya kawaida.

Kuhusu mpangilio wa maneno katika kamusi, inafahamika kuwa utaratibu uliozoeleka sana ni ule wa kialfabeti japokuwa upo pia ule wa kikoa maana. Hata hivyo mpango wa kialfabeti hauna budi kutazamwa kwa viwango viwili: Katika kiwango cha kwanza maneno hupangwa kwa kuzingatia herufi ya kwanza ya alfabeti ya neno. Kwa utaratibu huu maneno yote yanayoanza kwa herufi A huwekwa katika kundi moja. Vivyo hivyo kwa yale yenye kuanza na herufi B, CH, D ... hadi Z. Mpangilio wa kialfabeti wa kiwango cha pili ni ule wenye kuyapanga maneno ya herufi moja ya alfabeti kwa kuzingatia herufi ya pili, ya tatu, nne au tano ya neno kulingana na urefu wa neno. Mtumiaji wa kamusi ajuaye viwango hivi vya kialfabeti anaweza kupembua kamusi yake haraka na kupata neno analolitaka kwa kulitafuta katika herufi ya kwanza na kisha kuliangalia kwenye nafasi yake katika herufi yake ya pili, ya tatu na kuendelea hadi kulipata. Kinyume chake ingekuwa kulitafuta katika herufi ya kwanza na kisha kufungua kila ukurasa na kutazama kila neno hadi kulipata neno. Utaratibu huu humchukua mtumia kamusi muda mrefu sana kupata neno.

Kamusi ya lugha huwa na taarifa kuu sita: tahajia, matamshi, sarufi (mofolojia na sintaksia), maana, mifano ya matumizi na etimolojia. Kila taarifa

huweza pia kugawanywa katika kategoria ndogo ndogo ili kubainisha tofauti zilizomo baina ya maneno ya kategoria moja. Kwa mfano ndani ya kategoria nomino, kuna kategoria ndogo ya, ngeli za nomino (kwa Kiswahili) wingi wa nomino, za kuhesabika n.k. Vivyo hivyo kwa vitenzi. Kategoria ndogo ya vitenzi ni pamoja na uelekezi, vinnyambuo vya njeo n.k.Mpangilio wa taarifa nao ni mahsusi kwa kamusi kwani takribani kamusi nyingi zina mtiririko unaokaribiana katika kuwasilisha taarifa hizo hata kama kamusi nyingine zina taarifa nyingi au chache kuliko nyingine.

### **3.0 Wasemavyo Wanazuoni kuhusu Matumizi ya Kamusi**

Tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu matumizi ya kamusi na Barnhart (1962), Quirk (1973), Bejoint (1981), (1987) Herbst na Stein (1987) na Mdee (1997) zimeonyesha kuwa wanafunzi hutumia kamusi na kwamba wanaporejelea kamusi hutafuta baadhi ya taarifa zilizomo katika kamusi zao. Barnhart alitafiti wanafunzi wa vyuo huko Marekani na kubaini kuwa wengi wao walitafuta maana zaidi, kisha ikafuatia tahajia, matamshi, sinonimu, matumizi ya neno na etimolojia kwa mfuatano huo.

Quirk alitafiti tabia ya kutumia kamusi miongoni mwa wanafunzi wa chuo kikuu huko Uingereza baina ya wanafunzi wa masomo ya sayansi na sayansi za jamii, na pia miongoni mwa wanafunzi wa jinsia tofauti. Katika utafiti huu ilibainika kuwa wengi wa watafitiwa walimiliki kamusi zao wenyewe au nyumbani kwao kulikuwa na kamusi. Aidha, aligundua pia kuwa wengi wao walitumia kamusi kutafuta maana na tahajia za maneno zaidi.

Bejoint katika utafiti wake kuhusu matumizi ya kamusi kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya kigeni (Kiingereza) huko Ufaransa alibaini kuwa wanafunzi walikuwa hawajui kuwa kamusi zao zilikuwa na taarifa nyingi ambazo zilikuwa za manufaa kwao iwapo wangezitumia

Mdee naye katika utafiti wake alioufanya Chuo Kikuu cha York (Uingereza) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Tanzania) alitaka kujua taarifa wanazotafuta zaidi kwenye kamusi. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa wanafunzi wengi walitafuta maana zaidi kisha ilifuatia tahajia na jinsia ya maneno. Katika utafiti huo aliuliza pia iwapo wanafunzi walifundishwa jinsi ya kutumia kamusi yaani namna ya kutafuta neno katika kamusi na kutafsiri misimbo. Maoni ya watafitiwa yalikuwa kama ifuatavyo, zaidi ya asilimia 70 ya wanafunzi wa Kijerumani na Kifaransa huko York walisema hawakufundishwa jinsi ya kutumia kamusi ilihali karibu 60% ya wanafunzi wa Kifaransa wa Dar es Salaam walisema walifundishwa jinsi ya kutumia kamusi.

Matokeo ya tafiti zote hizi yanaonyesha kuwa wanafunzi hutumia kamusi. Lakini ni Bejoint pekee katika utafiti wake alidadisi stadi za kutumia kamusi na kagundua kuwa hawakuwa na stadi za kutosha kutumia kamusi na ndio maana hawakujua kuwa kuna taarifa zaidi ya maana katika kamusi zao ambazo zingekuwa za manufaa katika kujifunza Kiingereza kama wangezisoma.

Japokuwa Mdee alishughulikia kipengele hiki katika utafiti wake, hakuchunguza iwapo wana stadi za kutosha kuwawezesha kutumia kamusi kwa ufanisi. Maswali aliyouliza yaliwataka kueleza iwapo walifundishwa kutumia kamusi. Matokeo ya utafiti yanayotokana na maswali haya hayawezi kueleza iwapo wanajua jinsi ya kutumia kamusi kwani inategemea mambo waliyofundishwa na iwapo yanawatosheleza kuitumia kamusi kwa ufanisi. (Tazama Mdee 1997 katika LEXIKOS 7, 1997: uk 97). Isitoshe uchunguzi huu ulifanywa kwa wanafunzi wa Kifaransa wa Chuo Kikuu, hivyo kulikuwa na haja ya kujua iwapo wanafunzi wa shule za Sekondari na Msingi wanajua jinsi ya kutumia kamusi kwani katika viwango hivi matumizi ya kamusi kwa ajili ya kujifunza vipengele mbalimbali vya isimu na sarufi ya lugha ni muhimu sana.

Herbst na Stein (1987) wanasema kuwa ufundishaji wa lugha huko Ujerumani hauupi umuhimu mkubwa stadi za kutumia kamusi kwani inafikiriwa kuwa msomaji anaweza kudadisi na kupata maana ya kijuujuu ya neno kutokana na muktadha lilimotumika. Katika utafiti waliofanya kwenye vyuo vikuu vya Augsburg na Erlangen-Nuernberg wanafunzi 70 kati ya 160 walifahamu kuwa kamusi waliyokuwa wakiitumia ilikuwa na taarifa za kisintaksia kwenye ruwaza za vitenzi, na kwamba kati yao ni wanafunzi 26 tu ndio waliosema kuwa walifundishwa kuhusu ruwaza za vitenzi walipokuwa shuleni. Kwa mujibu wa watafiti hawa kikwazo cha kutofundishwa stadi za kutumia kamusi ni muda mchache utolewao kufundisha stadi hizi. Katika uchunguzi uliofanywa kwenye insha za mashindano ya kuandika insha kwa vijana wadogo katika lugha ya kigeni, imedhihirika kuwa makosa mengi ya tahajia na uundaji wa maneno wanayoyafanya yangeweza kuepukwa iwapo wanafunzi wangetumia kamusi. Kwa mujibu wa wanazuoni hawa, stadi za kutumia kamusi humsaidia mtu ajitegemee katika kutatua matatizo yanayomkabili anapojifunza lugha. Mwanafunzi anapokuwa na umilisi wa stadi hizi huweza:

- Kujua maana ya maneno
- Kuthibitisha tahajia ya neno
- Kufahamu namna ya kutamka neno
- Kumsaidia kupata maarifa mapya.

Kwa wanazuoni hawa stadi hizi huwa ni zana zinazomsaidia mtumia kamusi kuzifanya kwa ufanisi mkubwa shughuli zinazohusiana na utumiaji wa kamusi kama vile kusoma, kuandika, kutafsiri, kusikiliza n.k. Kutokana na hali hii wanaichukulia kamusi katika darasa la lugha kuwa ni mojawapo ya zana za kufundishia na ni sehemu ya kufundisha lugha yenyewe. Herbst na Stein wanakiri kuwa ingawa walimu wa lugha huitumia kamusi kama kifaa muhimu cha kufundishia hawawafundishi wanafunzi wao jinsi ya kutumia kamusi, na iwapo wakifanya hivyo hufundisha namna ya kutafuta neno tu, maarifa ambayo hayatoshi kabisa. Bejoint (1987) katika utafiti mwingine anasema kuwa kamusi zina taarifa nyingi ambazo zingewawezesha wanafunzi kujifunza lugha na

kupata taarifa nyingine za kiisimu, lakini kutojua jinsi ya kuitumia kamusi ndiko kunakowakwamisha wasiitumie kwa ukamilifu na kwa manufaa. Kushindwa huku kuitumia kwa ufanisi kunatokana na kutokuwa na stadi za kuitumia kamusi. Ili kuwaongezea stadi za kutumia kamusi anapendekeza kutayarishwe mwongozo wa namna ya kutumia kamusi ambao utawawezesha kupata stadi hizo.

#### **4.0 Mbinu za Utafiti**

Huu ulikuwa ni utafiti wa uwandani ambao uliwahusisha wanafunzi 43. Mbinu ya utafiti iliyotumiwa kukusanya data ni dodoso ambalo lilikuwa la mtindo wa jaribio lililokuwa na maswali manne ambayo mwanafunzi alitakiwa ayajibu kwa kadri alivyoweza. Mbinu hii ilitumiwa badala ya dodoso lenye maswali pamoja na majibu kadha ambayo mtafitiwa hutakiwa kuchagua jibu au majibu anayoona yanafaa. Mbinu hii imeonekana kuwa ina kasoro kwani haimpi mtafitiwa uhuru wa kutoa maoni yake kuhusu swali aliloulizwa kwa kuwa majibu tayari yameandaliwa.

Kasoro hii alieleza pia Hatherall (1984) alipohoji ubora wa matokeo ya utafiti unaotokana na maswali yenye majibu kwa kuuliza iwapo majibu watakayotoa watafitiwa yatakuwa : *mambo wanayoyafanya*, au *yale wanayofikiria kuwa wanayafanya* au *yale wanayofikiria kuwa wanapaswa kufanya* au *yote matatu*. Katika utafiti tuliofanya ambao matokeo yake yanawasilishwa katika sehemu ya 5.0 chini wanafunzi walipewa zoezi na sio dodoso lihusulo matumizi ya kamusi ambalo lililenga kuonyesha stadi za kutumia kamusi walizonazo wanafunzi waliofanya zoezi hilo.

#### **5.0 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data**

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kupima stadi za kutumia kamusi kwa wanafunzi wa sekondari. Wanafunzi waliulizwa maswali manne yaliyohusu utumiaji wa kamusi. Maswali hayo yalimtaka mwanafunzi:

- (1) kupanga maneno kwa mpangilio wa kialfabeti,
- (2) kutafuta maana za maneno katika kamusi ya lugha mbili,
- (3) kutafsiri misimbo ya leksikografia,
- (4) kutambua idadi ya maana za kidahizo

#### **5.1 Kupanga Maneno Kialfabeti**

Kati ya wanafunzi 43 ni wanafunzi wanne tu walioweza kupanga maneno yote kialfabeti kwa zaidi ya asilimia 50 ya maneno waliyopewa. Mwanafunzi 1 alipata 90% , mwingine alipata 80% na wengine wawili walipata 50% kila mmoja. Kati ya wanafunzi waliopata chini ya 50%, mmoja alipata 45% na mwingine 10%. Kwa kuangalia takwimu hizi inaonekana kuwa asilimia 9

walipata zaidi ya 50% na asilimia nyingine 4.6 ya wanafunzi walipata kati ya 10% – 45%. Hii ina maana kwamba wanafunzi wengi, yaani asilimia 86 hawakuweza kupanga maneno kialfabeti. Iwapo tungejumulisha wote wale ambao hawakupata 50% ya alama zilizotolewa kwa swali hili, ni dhahiri kuwa asilimia 91 ya waliohojiwa walishindwa kupanga maneno kialfabeti kama inavyoonekana katika jedwali 1 chini.

*Jedwali la 1: Uwezo wa wanafunzi kupanga maneno kialfabeti*

Wanafunzi	Alama
2.3%	90%
2.3%	80%
4.6%	50%
2.3%	45%
2.3%	10%
86%	0%

Japokuwa hawa ni wanafunzi wa kidato cha I ambao ndio kwanza wametoka shule za msingi, kushindwa huku kunaashiria kuwa wanafunzi wa shule za msingi hawajui kupanga maneno kialfabeti kwa kuzingatia herufi ya kwanza, ya pili na kuendelea hadi herufi ya mwisho ya neno. Japokuwa hii huweza kuashiria kutokuwa na mazoea ya kutumia kamusi, hali hii haitoshi kuhitimisha kuwa wanafunzi hawajatumia kamusi. Hali hii huweza kudokeza kuwa hawakufunzwa namna ya kuitumia kamusi kwa ufanisi. Kwa kuwa zoezi hili lilifanywa kwa muda maalumu, saa moja na nusu kujibu maswali manne, ni dhahiri kuwa wengine walishindwa kuyapanga upesi kadri inavyotakiwa kwa muda waliopewa.

## **5.2 Kutafuta Maana za Maneno**

Kuhusu kutafuta maana za maneno, wanafunzi walipewa orodha ya maneno pamoja na kamusi ya lugha mbili Kiswahili – Kiingereza na kutakiwa kutafuta maneno hayo katika kamusi na kunakili maana au kisawe kimoja tu kutoka katika kamusi. Lengo la jaribio hili lilikuwa kupima uwezo wao wa kutafuta neno katika kamusi na kubaini maana kati ya taarifa nyingine zilizomo. Matokeo ya zoezi hili yameonyesha kuwa wanafunzi wengi waliweza kutafuta neno na kisha kunukuu kisawe chake kimoja kama ilivyoagizwa. Asilimia 44 ya wahojiwa wote walijibu swali kwa usahihi na kupata alama zote (100% za alama za swali hili.) Asilimia 51 walipata alama kati ya 50% - 95% ilihali asilimia 5 ndio ambao walishindwa kama jedwali la 2 linavyotuonyesha.

Wanafunzi	Alama
44%	100%
28%	90%
2.3%	85%
11.6%	80%
2.3%	70%
4.6%	60%
2.3%	50%
2.3%	13%
2.3%	0%

Ufanisi bora katika kujibu swali hili unaweza kuelezwa kuwa unatokana na welewa wa watu wengi kuhusu kamusi kuwa ni kitabu cha maneno na maana zake. Hii inaonyesha kuwa wanafunzi hawa wamekuwa wakitumia kamusi kutafuta taarifa hii. Aidha, ufanisi huu unashadidia matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa kuwa maana ndiyo taarifa inayotafutwa na watumiaji wengi wa kamusi na kwamba wanafunzi huirejelea kamusi ili kutafuta taarifa hii. Tazama 3.0 juu.

### 5.3 Kutafsiri Misimbo iliyo katika Kamusi

Swali kuhusu lugha ya kamusi (lugha kienzo ya kamusi) bila shaka limeelekea kuwatatiza wahojiwa. Swali hili liliwataka wafafanue maana ya misimbo iliyowekwa mkabala na vidahizo ambayo huwakilisha taarifa fulani za kileksikografia zinazokihusu kidahizo husika katika kamusi ya Kiswahili. Misimbo hii ni: a) *ku*, b) *kt*, c) *ji*, d) *kl*, e) *kv* na f) *vi*-. Ufafanuzi uliotakiwa ulikuwa ni kueleza kirefu cha kifupisho kinachounda misimbo hiyo. Mbali na kuifafanua, walitakiwa pia kueleza dhima ya kila moja kwa kidahizo kinachohusika. Matokeo yake yanadhihirisha kutoelewa lugha itumiwayo katika kamusi. Inatosha kueleza hapa kuwa *ku* (kiunganishi), *kt* (kitenzi), *ji* (jina), *kl* (kielezi), *kv* (kivumishi) na *vi*- (kiambishi wingi cha ngeli ya ki-) ambacho kwa pamoja huunda ngeli ya [ki-/vi-]. Kwa hivyo misimbo a) – e) inaashiria kategoria za kisarufi kwa kila kidahizo ambapo msimbo umewekwa, yaani: *na ku*, *babaisha kt*, *babu ji*, *badala kl* na *badilifu kv*. Msimbo wa f) *vi*- ni kiambishi awali cha wingi cha nomino yenye kuanza na kiambishi *ki*-mathalani *kigwe*, *vigwe*. Matokeo ya swali la lugha kienzo yanaonyesha kuwa hakuna mhojiwa aliyeweza kujibu swali kwa usahihi na kupata zaidi ya asilimia 50 ya alama. Ni asilimia 4.7 ya wahojiwa waliweza kufafanua misimbo hii kwa 33%, asilimia 9 walipata 27% ya alama, wengine asilimia 4.7 walipata alama 20% na asilimia 9 nyingine walipata alama 7%. Wahojiwa walio wengi (yaani 69%) hawakuweza kufafanua msimbo wowote. Jedwali la 3 linadhihirisha haya.

### Jedwali la 3: Kutafsiri misimbo ya leksigografia katika kamusi

Wanafunzi	Alama
4.7 %	33 %
9.3 %	27 %
4.7 %	20 %
9.3 %	7 %
69.7 %	0 %

Matokeo haya yanaonyesha upekee wa lugha ya kamusi. Ingawa wanafunzi hawa wanatarajiwa kuwa wamefunzwa aina za maneno na ngeli za nomino, matumizi ya vifupisho vya kategoria hizi ambazo hutumika tu katika kamusi ndiyo yaliyowatatiza. Laiti kategoria hizi zingeandikwa kwa kirefu yaani *nomino*, *kitenzi*, *kivumishi* n.k. huenda wanafunzi wangeelewa na kueleza dhima za kila moja katika neno linalolihusu.

#### 5.4 Kutambua Idadi za Maana za Kidahizo

Swali la nne liliwataka wahojiwa kutafuta maana za maneno waliyopewa kutoka katika kamusi na kisha kuandika idadi ya maana zilizomo kwa kila kidahizo, kunakili maana ya mwisho ya kila kidahizo. Swali hili lilipima mambo matatu:(1) kutambua maana, (2) kubaini idadi ya maana, na (3) kutambua msimbo wa homonimu kwani kidahizo kimojawapo kilikuwa ni homonimu. Itafaa kusisitiza hapa kuwa maana ya neno ni maelezo yenye sifa bainifu za kisemantiki za neno ambazo zatosheleza kutofautisha maana ya neno moja na maana ya maneno mengine yenye kushiriki kiko maana kimoja. Kidahizo chenye maana zaidi ya moja hubainishwa kwa tarakimu inayoitangulia maana husika ikianza na tarakimu '1'. Kwa hivyo kidahizo chenye maana mbili au tatu, maana hizo zitadhihirishwa kwa tarakimu zinazotangulia maana hizo. Lakini kidahizo chenye maana moja tu hakiashiriwi. Ishara ya homonimu iliyotumika katika kamusi hii ni herufi kubwa ambayo huwekwa katika mabano ya mraba mathalani [A], [B], [CH] n.k. baada ya kidahizo. Kwa mfano, babu [A], babu [B], babu [CH], babu [D] na babu [E]. Ishara hii hutumiwa kubainisha vidahizo vyenye umbo linalofanana lakini bila kuwa na uhusiano wa kimaana wala kietimolojia.

Matokeo ya data hii yanaonyesha kuwa asilimia 4.6 ya wahojiwa wote waliweza kutafuta kidahizo katika kamusi, kutambua idadi ya maana na kunakili maana ya mwisho. Karibu asilimia 20 waliweza kupata alama zaidi 50% za swali hili. Wahojiwa wengine asilimia 25.6 walipata alama kati ya 30% - 39%. Waliopata alama za chini kabisa yaani chini ya 30% ya alama za swali hili ni wahojiwa 46% kama jedwali la 4 linavyoonyesha:



*Jedwali la 4: Kutafuta maana na kubainisha idadi yake*

Wanafunzi	Alama
4.6%	89 %
7.0%	79 %
7.0 %	50 %
9.3 %	44%
14.0 %	39 %
2.3 %	33 %
2.3 %	28 %
14.0 %	22 %
2.3 %	16 %
4.6 %	10 %
32.6 %	0 %

Kwa kuangalia data nzima tunapata picha ya jumla kuhusu jaribio hili ambayo twaweza kuitumia kusawiri jedwali la tano linaloonyesha wastani wa ufanisi kwa kuzingatia maswali yote kwa pamoja.

*Jedwali la 5: Kiwango cha umilisi wa stadi za kutumia kamusi*

Wanafunzi	Alama
2.3 %	74 %
2.3 %	60%
16.3 %	40 – 49 %
27.9%	30 – 39 %
37.4 %	20 – 29 %
11.6 %	10 – 19 %
2.3 %	0 – 9 %

Picha ya jumla inayojitokeza katika mchanganuo huu wa data ni kwamba wanafunzi wa Sekondari wanao umilisi mdogo wa stadi za kutumia kamusi. Ni asilimia 4.6 yao tu ndio walioweza kupata wastani wa jumla ya alama zaidi ya 60% ya alama za jaribio hili la kileksikografia yaani wanaweza kupanga maneno kialfabeti, na kwa hali hii huweza kufanya yafuatayo: a) kutafuta maneno yaliyopangwa kwa kuzingatia mpango wa kialfabeti, b) kutafuta maana na kubaini idadi yake, c) kutafsiri misimbo iliyotumika kuwasilisha taarifa za leksikografia. Asilimia nyingine 16.3 inaonyesha kuwa inajuajua kutumia kamusi. Hawa ni wale waliopata wastani wa alama 40-49%. Waliobaki wote ambao ni sawa na asilimia 79 hawana stadi za kutumia kamusi kabisa. Kwa kuzingatia wingi huu wa wasiojua kuitumia kamusi, twaweza kusema kuwa stadi za kutumia kamusi hazijulikani kwa wanafunzi wa sekondari wa

kidato cha kwanza. Sababu kadha zinaweza kuhusishwa na kutofahamika huku kwa stadi za kamusi. Baadhi ya sababu ni kama zifuatazo:

1. *Wanafunzi kutokuwa na kamusi za kutumia.*

Tabia ya kutumia kamusi hujengeka iwapo mwanafunzi ana kamusi yake mwenyewe au ya shule ambayo hupata fursa ya kuitumia awapo shuleni. Hali kadhalika tabia hii hujengeka pia iwapo familia humiliki kamusi majumbani kwao. Kwa kutumia kamusi wangeweza kujifunza namna ya kuitumia kwa kujisomea wao wenyewe utangulizi na kupata maarifa hayo japokuwa haitowapatia stadi zote kwani nyingine hazimo kwenye kamusi. Aidha wangeweza kufundishwa stadi hizi na walezi au ndugu zao huko nyumbani. Iwapo familia wanakotoka wanafunzi hawa haina kamusi watakosa pia umilisi wa kuitumia kamusi.

2. *Wanafunzi wenyewe kutotumia kamusi.*

Baadhi ya shule huwa na kamusi, lakini kutokana na sababu kadha, mathalani walimu kutotaka wanafunzi watumie kamusi ili wajifunze kutambua maana kutokana na mktadha. Halikadhalika tabia ya kupenda kuzitunza kamusi zisichakae na kuzihifadhi kwenye kabati ili wanafunzi wasizitumie isipokuwa walimu; nayo huwanyima wanafunzi fursa ya kuzitumia .

3. *Kutofundishwa stadi hizi katika somo la lugha*

Walimu wengi hawajui umuhimu wa kamusi kwa mwanafunzi wa lugha mbali na kuitumia kupata maana ya maneno. Kutokana na hali hii wanafunzi huelekezwa tu kutafuta neno kwa kuzingatia herufi ya kwanza ya alfabeti ya neno. Maarifa haya hayatoshi kuitumia kamusi kwa ufanisi.

4. *Walimu kutojua stadi za kutumia kamusi*

Walimu ni zao la jamii isiyotumia kamusi wala kufundishwa jinsi ya kuitumia. Kwa hali hii wao wenyewe hawana stadi za kufundisha wanafunzi wao.

5. *Kutokuwa na kiongozi cha stadi za kutumia kamusi*

Somo linalohusu stadi za kutumia kamusi ni geni. Mambo machache sana yanafahamika kwa walimu. Walimu wangeweza kufundisha stadi hizi iwapo kungekuwa na kiongozi au kitabu chenye mada zinazohusu somo hili ambacho walimu wangejisomea na kuwafundisha wanafunzi wao.

6. *Muhtasari wa lugha kutokuwa na kipengele cha "Matumizi ya kamusi"*

Ufundishaji wa stadi za kutumia kamusi ungechochewa na kuwapo kwa mada hii katika muhtasari wa somo la Kiswahili, pamoja na kutengwa muda wa kufundisha mada zinazohusu matumizi ya kamusi. Kuwepo kwa muhtasari na muda wa kufundisha kungewahamasisha walimu kutafuta matini za kufundishia. Matokeo ya utafiti huu hayana budi kuchochea haja ya kufundisha stadi hizi shuleni.

## 6.0 Stadi za Kutumia Kamusi

Tumekwisha kuona kuwa tunaweza kuitumia kamusi kwa ufanisi iwapo tunajua stadi za kuitumia. Kwa hivyo ili kufanikisha hili hatuna budi kufundisha stadi hizi. Kuweza kuzifundisha ni muhimu kwanza kuifahamu kamusi, sehemu zake kuu na maudhui ya kila sehemu. Pili ni muhimu kujua mpangilio wa vidahizo katika kamusi, taarifa zilizoingizwa katika kamusi na namna zilivyoingizwa. Kamusi za wanafunzi wa viwango tofauti hutofautina kwani huwa na maudhui tofauti. Kwa hali hii stadi za kutumia kamusi hazina budi kuzingatia kiasi cha maudhui kilicho katika kila kamusi. Kwa kuwa elimu ya sekondari hutegemea sana msingi uliowekwa katika elimu ya msingi, stadi za kutumia kamusi kwa kiwango hiki lazima zijikite kwenye stadi za kamusi za elimu ya msingi. Kutokana na hali hii ni muhimu kwanza kubainisha stadi za kamusi kwa wanafunzi wa elimu ya msingi.

### 6.1 Stadi za Kamusi kwa Wanafunzi wa Elimu ya Msingi

Kamusi za wanafunzi wa elimu ya msingi zina mambo manne muhimu:

- a) Mpango wa kialfabeti.
- b) Sarufi,
- c) Maana,
- d) Mifano ya matumizi.

Kwa kuwa maneno yamepangwa kialfabeti ni muhimu kufundisha jinsi maneno yanavyopangwa kialfabeti kwa kuzingatia mpango wa alfabeti wa herufi ya kwanza, ya pili na kuendelea kulingana na urefu wa neno. Utaratibu huu utawasaidia kutafuta neno katika kamusi. Kiwango cha sarufi kwa wanafunzi wa msingi ni kidogo kwani kinahusu nomino za wingi kwa kila nomino ya umoja. Kwa mfano, *mtoto – watoto, kiti – viti, embe – maembe, uzi – nyuzi* au *child – children, ubao – mbao, chair – chairs, mango – mangoes, thread – threads* n.k. Wanafunzi wa kiwango hiki hawaonyeshwi kiambishi cha wingi cha nomino kwani ni dhana wasizozijua ambazo ni ngeni kwao na zinaweza kuwa ngumu. Kwa kamusi ya Kiingereza vitenzi huhitaji pia vinyambuo kwa njeo tofauti, mathalani, *drink (drinks, drinking, drunk, drank)*. Maelezo ya maana hufuata taarifa ya kisarufi. Maana hubainishwa kwa tarakimu ambayo hutangulia maana iwapo neno lina maana zaidi ya moja. Tarakimu hudokeza idadi ya maana za neno. Maana hufuatwa na mifano ya matumizi ambayo ni tungo yenye kuonyesha namna neno linavyotumika katika lugha ya kawaida watu wanapozungunza. Mfano wa matumizi hufuata maana ya neno.

Maelezo yakitolewa kwa mpangilio huo na kufafanuliwa na mifano halisi kutoka katika kamusi, wanafunzi wataelewa na kupata umilisi wa stadi za kutumia kamusi ya kiwango chao. Stadi hizi ni msingi kwa madarasa ya juu kwani mambo waliyoyaona hapa hujitokeza pia katika kiwango cha juu isipokuwa baadhi hupanuka zaidi. Inafaa basi ikumbukwe kuwa katika kiwango

hiki istilahi za sarufi kama vile nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi n.k. au zile za leksikografia kama vile kitomeo au kidahizo hazitumiwi katika maelezo wala kuonyeshwa katika kamusi zao.

## 6.2 Stadi za Kamusi kwa Wanafunzi wa Sekondari

Wanafunzi wa sekondari watajifunza mambo yafuatayo:

- a) Mpango wa kialfabeti
- b) Matamshi ya maneno
- c) Sarufi : kategoria ya kidahizo huonyeshwa, kisha viambishi vya wingi, vipatanishi vya kisarufi baina ya nomino (katika kiima) na kitenzi (iliyo katika kiarifu, kwa kamusi ya Kiswahili), vinyambuo vya vitenzi na vinyambuo vya njeo za vitenzi (kwa kamusi ya Kiingereza) na ruwaza za virai vitenzi.
- d) Maana za vidahizo: sinonimu (iwapo kamusi ni ya lugha mbili) na sinonimu au fasili (iwapo kamusi ni ya lugha moja) na jinsi zinavyotengwa
- e) Mifano ya matumizi
- f) Etimolojia ya neno: Ishara za kudokeza etimolojia pamoja na lugha chasili au lugha mbalimbali neno lilimopitia hadi kuingia lugha lengwa huonyeshwa.
- g) Matumizi ya lugha kwa mujibu wa mazingira lugha inapotumika: rasmi au sirasmi, lugha ya mitaani, lugha ya utani, hadhi ya maneno kama vile tasfida, matusi au kizamani n.k..

Katika kiwango hiki istilahi kadha zitatumika kwani wanafunzi hawana budi kuanza kudokezwa dhana za taaluma ya lugha na leksikografia. Wanafunzi wafundishwe mada hizi kwa kutumia mifano kutoka kwenye kamusi. Mada zilizobainishwa kwa kila kiwango cha elimu zitahitaji muda wa kuzifundisha. Kwa hivyo haitarajiwi kuwa mada hizi zitafundishwa katika kipindi kimoja. Kwa kuwa mada hizi ni muhimu kwa mwanafunzi kuzijua ili aweze kuitumia kamusi kwa ufanisi, zinahitaji muda wa kutosha wa kuzifundisha. Kwa hali hii ni dhahiri kuwa mwalimu hana budi kuzipatia mada hizi nafasi katika vipindi vyake vya lugha. Aidha watunga mitaala inawabidi sasa kutafakari uwezekano wa kuandaa muhtasari wa lugha utakaoingiza mada zinazohusu stadi za kutumia kamusi katika somo la Kiswahili na Kiingereza pia.

## 7.0 Hitimisho

Makala yamejadili umuhimu wa kutumia kamusi kama nyenzo ya kufundishia lugha. Katika mjadala huu imeonyeshwa kuwa matumizi ya kamusi yenye ufanisi yanahitaji stadi za kutumia kamusi. Kwa kutumia data iliyotokana na utafiti wa uwandani imedhihirika kuwa wanafunzi hawana stadi za kutosha kuwawezesha kutumia kamusi kwa ufanisi. Kutokana na mjadala huu

imehitimishwa kuwa ni muhimu stadi hizi zifundishwe kuanzia elimu ya msingi hadi sekondari. Ili kuwapa changamoto walimu wa lugha na wakuza mitaala, mapendekezo ya mada za stadi za kutumia kamusi yametolewa kwa kila kiwango. Aidha, imependekezwa pia kuwa walimu wa lugha watenge muda wa kufundisha stadi za kutumia kamusi, na Taasisi ya Elimu ya Tanzania iandae muhtasari wa lugha ambao utajumuisha kipengele cha Stadi za Kutumia Kamusi.

Mwisho tungependa kusesitiza kuwa japokuwa utafiti huu umehusisha wanafunzi wachache, umedhihirisha hali ya matumizi ya kamusi shuleni. Hata hivyo kuna haja ya kufanya utafiti mpana zaidi utakaohusisha wanafunzi wengi zaidi na wa madarasa tofauti, shule zaidi na mawanda zaidi ya kuchunguza. Aidha, ingefaa pia kupata maoni ya walimu pia.

### Marejeo

- Barnhart, C. L., (1962), "Problems in Editing Commercial Monolingual Dictionaries". In *Problems in Lexicography*, Fred W. Household and Sol Saporta (Eds) Indiana Research Center in Anthropology, Folklore, and Linguistics
- Bejoint, Henri, (1981), "The Foreign student's Use of Monolingual English Dictionaries: a Study of Language Needs and Reference Skills", *Applied Linguistics* 2, 3 ; 207 – 222
- Bejoint Henri na Andre' Moulin (1987) The Place of a dictionary in an ELF programme. In *The Dictionary and the Language learner*, Anthony Cowie (Ed).
- Cowie A., (1987), (Ed) *The Dictionary and the Language Learner*. LEXICOGRAPHICA series Papers from EURALEX seminar at the University of Leeds 1-3 April 1985 Max Niemeyer Verlag, Tuebingen
- Hatherall, G., Studying Dictionary use: Some Findings and Proposals. In Hartmann R.R.K (Ed) *1984 Lexeter Proceedings* .
- Herbst T. and Gabriele S., (1987), Dictionary Using Skills: A plea for a new orientation in Language Teaching. In Cowi A. (Ed) *The Dictionary and the Language Learner*
- Mdee, J.S.,(1997), Language Learners' Use of a Bilingual Dictionary: A comparative Study of Dictionary Use and Needs. In LEXIKOS 7 1997 BURO VAN DIE WAT
- Quirk, R. (1973) "The Social Impact of Dictionaries in the UK" In *Lexicography in English*. Raven I. McDavid and Audrey R. Duckert (Eds)